

**SHULE YA UPILI YA GATITU**  
**MTIHANI WA KATI YA MUHULA WA TATU**  
**KIDATO CHA KWANZA 2015**  
**KISWAHILI**

**1)UFAHAMU**

**SOMA KIFUNGU KIFUATACHO KISHA UJIBU MASWALI**

Vijana ni tegemeo kubwa kwa kila taifa na bila shaka wao ni viongozi wa kesho kama ilivyo msemu wa kawaida. Isitoshe, takwimu za idadi ya watu nchini Kenya zinaonyesha kuwa idadi ya vijana inachukua asilimia sitini hivi, hii ikiwa ni sehemu kubwa ya wapigaji kura ambao uamuzi wao hutupa viongozi, wanasiasa wema na wabaya. Ndiposa kila taifa lenye masomo ya kuwa na maendeleo, lazima liweze kutambua umuhimu wa vijana ambao ni asasi muhimu ya maisha na viongozi wa kesho. Serikali imejaribu kuanzisha miradi mbalimbali humu nchini kwa minajiri ya kuwainua vijana.

Tumeona kazi kwa vijana na kulifurahia wazo nzuri la serikali kuona kwamba vijana wanapata kazi na pato japo kidogo. Lakini mbona ufidadi na ufujaji wa pesa kama hizi umekuwa kama sumu ya kuharibu kilicho kizuri?Tungependa kuona vijana wakishirikishwa katika utendakazi badala ya kukaa hivi hivi mitaani pasi na kufanya lolote,si mapenzi ya wakenya kuwaona vijana **wakiogelea kwenye dimbwi la vileo** na dawa za kulevya.

Taifa letu linawahitaji vijana, siyo tu kwa kutumiwa **kuwapigia debe** vigogo wa kisiasa lakini tunawahitaji kama **mihimili** muhimu ya viongozi wa kesho.Simba akikosa nyama,tumesikia kuwa yeye hula nyasi na mtoto

akikosa la mama hata la mbwa huamwa.

Ukosefu wa kazi na hasa kwa vijana umekuwa kama **limbukizi la makaaa kwenye tanuri la matatizo** kwa vijana na kwa kukosa matumaini, wengi wa vijana wamejitosa kwenye ulevi wa kila aina ya vileo, bora tu mtu ajihisi kuwa yupo mbingu ya tatu kama si ya nne. Hali ya maisha ya vijana imekuwa si hali tena na hasa vijana wanaume. Kwa wale wameoana wamebaki tu kuwa picha kwenye ndoa zao, ulevi **umetamalaki** maisha yao hivi kwamba hata kupata watoto ni kama tu kupanda mchongoma.

Kaunti mbalimbali za Kenya zinalia, mabibi wakiwalilia waume wao. Kila siku imekuwa ni siku ya maandamano, wakiandamana kwa sababu ya pombe haramu ambazo zimewaoa waume zao na kuwafanya watumwa na si watumwa tu lakini watumwa hanithi ambao hawawezi kupata watoto katika hali zao. Inafedhehesha kuona hata nyumba nyingi zinaongozwa na kutunzwa na mabibi.

Hivyo basi kilichobaki ni wakenya wote kwa jumla kuendeleza na kuunga mkono sheria ya Mututho, ili tuwaokoe viongozi wa kesho. Asiyesikia la mkuu mwishowe ...

### Maswali

- a) Eleza matatizo yanyokumba juhudi za kuwainua vijana. (alama 3)

---

b) Kulingana na mwandishi, kwa nini ni muhimu kuwashughulikia vijana?  
(alama 2)

---

c) Mwandishi anamaanisha nini kwa kusema, limbikizi la makaa kwenye tanuri la matatizo? (alama 2)

---

d) Kwa vijana ambao ni waraibu wa ulevi, kupata watoto ni kama tu kupanda mchongoma. Eleza (alama 2)

---

e) Andika methali mbili zilizotajwa kwenye kifungu . (alama 2)

---

f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika kifunguni (alama 4)

i) wakiogelea kwenye dimbwi la vileo

---

ii) kuwapigia debe

---

iii) mihimili

---

iv) Pombe haramu ipigwe marufuku

---

## 2.MATUMIZI YA LUGHA

a)Eleza sifa mbili mbili a konsonanti hizi:

i) /p/

(al 4)

ii) /z/

b)Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa

(al 2)

Uso wa mwanamke yule ulichujuka alipoanguka

c)Sahihisha sentensi ifuatayo.

(al 2)

maji iliyowekwamtungini imemwagika

d) Bainisha maneno katika sentensi zifuatazo.

(al 5)

i)Lo! Majambazi wengi wamewavamia wanakijiji usiku

ii)Wewe usitembee katikati ya barabara

e)Geuza sentensi hii katika nafsi ya tatu

(al. 1)

Mimi nitaenda mjini kesho

f)Tumia “amba” kuunganisha sentensi hizi.

(al. 1)

Shamba limenunuliwa . Shamba litapandwa pareto

g) Andika upyasentensi hizi katika kauli zilizo mambanoni

(al. 2)

i) motto alikimbia kwa mama (kutendewa)

ii) Omolo amekopa pesa za Wafula (kutendesha)

h) Maneno haya yako katika ngeli gani ?

(al. 3)

i) choo

ii) hasira

iii) ugonjwa

i) Taja visawe vya maneno haya.

(al. 2)

ruhusa

ii) fikiri

j) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi ya mshazari (/)

(al. 2)

k) Fafanua sifa mbili za lugha ya shuleni

(al. 2)

3) FASIHI SIMULIZI

ai) Misimu ni nini ?

(al. 1)

ii) Eleza sifa nne za misimu

(al. 4)

---

---

---

---

---

---

---

b) vitendawili vina umuhimu gani katika jamii?

(al. 4)

---

---

---

---

---

---

---